OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG
SHULE YA SEKONDARI ENDASAK - S.L.P. 145 – KATESH/HANANG

Simu: 0788744141
0786497695

Kumb. Na. ED/ESS/J.I/VOL.I/119 Tarehe: **1/12/2020**

Mwanafunzi: ……
S/M …….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ENDASAK – WILAYA YA HANANG' – MWAKA 2020:

1. **UTANGULIZI:**
   Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2020 katika shule ya Sekondari Endasak. Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2020,** hivyo unatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa au kuchelewa saa 1.30 asubuhi kwa tarehe iliyotajwa.
   Agizo muhimu: Unatakiwa kuwa darasani tarehe 11/1/2020 tayari kwa masomo, hivyo zingatia muda wa kufanya maandalizi mapema.
2. **MAMBO YA KUZINGATIA:**
   2.1: Sare ya shule:
   2.1.1. Nguo: Kila mwanafunzi ajinunulie sare zake kama ifuatavyo:-
   (a) Wasichana: (i) Sketi mbili nyeusi za marinda 12 ndefu mpaka kwenye jicho la mguu na 'belt' ndogo.
   (ii) shati mbili nyeupe mikono mifupi.
   (iii). Sweta mbili shingo 'V' kijani-jeshi.
   (iv). Nguo za michezo – 'Tracksuit' nyeusi yenye ufito mweupe pembeni
   (b) Wavulana:
   (i) Suruali mbili rangi nyeusi zenye rinda mbili kila upande, mfuko 1 nyuma na miwili mbele, **mzunguko wa chini inchi '8';** isiwe na mtindo wa jinsi.(miguu kubana chini).
   (ii) Shati mbili nyeupe mikono mifupi.
   (iii). Sweta mbili shingo 'V' kijani-jeshi.
   (iv). Nguo za michezo – bukta na fulana (T-shirt) rangi ya bluu.

   2.1.2 Sare zingine kwa wote:
   i. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba – jozi mbili.
   ii. Fulana (T-shirt) 1 yenye nembo ya shule (maelekezo utapewa shuleni).
   iii. Raba za michezo.
   iv. Socks ndefu jozi mbili, khaki wavulana na nyeupe wasichana.

   2.2**. Mahitaji mengine muhimu:**
   i. Daftari kubwa 12 za kuanzia (counter books Quire 2).
   ii. Kamusi ya Kiingereza (Dictionary).
   iii. Vitabu vya kujifunzia.
   iv. Kalamu za wino na penseli.
   v. Rula na kifutio (raba)
   vi. Mkebe wa Hisabati uliokamilika (complete mathematical set).
   vii. Vyombo vya chakula, sahani 1, kijiko na kikombe – aluminium au mfupa (visiwe vya plastiki)
   viii. Rimu moja A4 kwa ajili ya mazoezi na majaribio mbalimbali

   2.3. **Huduma ya chakula shuleni: (Inasimamiwa na kamati ya wazazi):**
   Kuchangia nafaka; mahindi masafi debe 4 na maharage debe 2 kwa mwaka (aina yoyote) – isipokuwa maharage ya farm na meusi, fedha Tsh. 20,000/= kwa muhula (40,000/= kwa mwaka), fedha hizo ziwekwe benki ya **NMB A/C Na. 41010006286,** Jina la akaunti; **KAMATI YA CHAKULA ENDASAK** SEKONDARI na risiti ya benki iwasilishwe shuleni. Mzazi/mlezi atakayeleta fedha shuleni **hazitapokelewa.**

NB: Mwanafunzi atakayeripoti shuleni bila kuletwa na Mzazi/Mlezi hatasajiliwa.

…….
MKUU WA SHULE:

SHERIA ZA SHULE:

A: HESHIMA:

(i) Wanafunzi wawe na heshima kwa walimu, wafanyakazi wote wa shule, wao kwa wao na mtu mwingine yeyote anayewazidi umri.
(ii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wote kati yao wenyewe, kwa walimu wao na kwa watu wengine.
(iii) Wanafunzi wote ni lazima washirikiano na kusaidiana na waheshimu na kuthamini kazi za aina zote.
(iv) Wanafunzi wote hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-
  (a) Kuvuta sigara, bangi na kutumia madawa ya kulevya,
  (b) Kunywa pombe,
  (c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima,
  (d) Kugombana.
(v) Wanafunzi wanatakiwa kuitikia mara moja na kukimbilia wanakoitwa.
(vi) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu Bendera ya serikali, picha za viongozi wa serikali, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
(vii) Wanafunzi waheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za shule, kutunza na kuthamini mali binafsi na mali ya umma.
(viii) Wanafunzi wawe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote walipo.
(ix) Wanafunzi wawe kimya wakati wote wakiwa darasani, wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
(x) Wanafunzi wanyoshe mkono juu na wasimame wanapoulizwa na kujibu maswali.
(xi) Uhusiano kati ya wavulana na wasichana **uwe wa kimasomo tu.**

B: MAHUSIANO:

(i) Ni lazima wanafunzi wote wahudhurie vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
(ii) Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie kazi zote za mikono.
(iii) Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa.
(iv) Kwa kuzingatia sheria ndogo ya mahudhurio ya lazima katika shule za sekondari Wilayani Hanang – Mwanafunzi atakayekosa/acha shule **BILA SABABU YA MSINGI** pamoja **mzazi/mlezi** atakayesababisha mwanafunzi kuacha shule/ masomo atachukuliwa hatua **za KISHERIA KWA KUZINGATIA SHERIA NDOGO HIYO**.

C: KUWAHI;

(i) Wanafunzi wote ni lazima wawahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku, kama vile vipindi vya darasani na nje ya darasa, wakati wa zamu, kurudi shuleni baada ya likizo n.k.
(ii) Wanafunzi ni lazima kuwahi haraka wanaosikia wito wa dharura.

D: SARE YA SHULE:

(i) Ni lazima wanafunzi wote wavae sare ya shule wakati wote wa:-
  (b) Masomo ya darasani,
  (c) Wanapotoka nje kwa shughuli za kishule.
  (d) Mhadhara wa shule (Baraza).
  (e) Wanapokwenda Hospitalini.
  (f) Maandamano rasmi.
  (g) Wanapokuja shuleni na kurudi nyumbani jioni.
  (h) Kofia, viatu vya ghorofa na mapambo yoyote haviruhusiwi kuvaliwa na sare.
  (i) Usafi was are na mavazi yote yaliyoruhusiwa kuvaliwa shuleni uzingatiwe kwa kila hali.

E: MIPAKA YA SHULE:

(i.) Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ya kibali/ruhusa maalum na warudi kwa saa zilizoruhusiwa/kupangwa.
(ii.) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila ya kibali maalum:-
  (a) Ofisi ya shule.
  (b) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.
  (c) Vilabu vya pombe.
  (d) Majumba ya starehe.
  (e) Nyumba za kulala wageni.

NB: C,D NA E – Hakuna kibali kinachotolewa.

F: USAFI:

i. Kila mwanafunzi ni lazima azingatie usafi wa vifaa vyote anavyotumia hapa shuleni, usafi wake binafsi kama vile mwili, sare n.k.
ii. Kila mwanafunzi ni lazima awajibike kwa usafi wa mazingira ya shule, ni marufuku kutupa makaratasi ovyo, na pia ni marufuku kupita njia za vichochoro; kila mwanafunzi lazima atunze bustani za maua kwa kila hali n.k.

- Wanafunz kike waje na ndoo moja ya lita 10 na fyekeo moja kwa ajili ya usafi.Wavulana waje na ndoo ndogo moja ya lita 10 na mopper moja.

G: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI:

1. Wizi,
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulvi na matumizi ya madawa ya kulevya.
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa.
9. Kuolewa/kuoa.
10. Kupata mimba/kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa/kuharibu mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

MUHIMU (TANBIHI): Adhabu kwa uvujaji wa sheria za shule zitatolewa na Baraza la walimu, Bodi ya shule na vyombo vingine vinavyohusika.

****

SHULE YA SEKONDARI ENDASAK

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE:

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Endasak,
S.L.P. 145,
KATESH – HANANG,
MANYARA.

A: MWANAFUNZI:

Mimi ……..nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule yako. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninaikubali*/ninaikataa nafasi hiyo kwa sababu ……..
Pia nayakubali*/nayakataa masharti na sheria za shule yako. Ninaahidi kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai; makosa kama hayo yanasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule. Hivyo nikishiriki makosa hayo nifukuzwe shule.

…… …….
Tarehe Saini

B: MZAZI/MLEZI:

Mimi ……..mzazi*/Mlezi wa …… ambaye amechaguliwa kujiunga na shule yako. Nimesoma maagizo ya kujiunga na shule yako na ninakubali*/ninakataa nafasi hiyo. Ninaahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule yako katika muda uliopangwa, pia nitashirikiana daima na shule yako katika kumkuza mtoto na kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake, wazazi na Taifa kwa ujumla. Kama unakataa toa sababu:
……
……
Ninaahidi mwanangu kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Mwanangu akishiriki makosa hayo afukuzwe shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi …… Tarehe ……..

NB: Udanganyifu wowote ambao utasababisha/lenga kumkosesha mwanafunzi masomo/shule hautavumiliwa.

Ahsante,

Jina na anwani ya Mzazi/Mlezi:
……
……
……
Namba ya simu ……

*Futa lisilohusika.

(Tafadhali uje na fomu hii ikiwa imejazwa vizuri)

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY
ENDASAK SECONDARY SCHOOL *** P.O. BOX 145 * KATESH/HANANG' – MANYARA**

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION:
To be completed by a Government Medical Officer.

Pupil full name ……
Age: ……
Blood count (Red and white) ……
Stool examination ……
Urinalysis: ……
Syphilis Test ……
T.B. test ……
Eye test ……
Ears ……
Chest ……
Spleen ……
Abdomen ……

Additional information: e.g. Physical defects or impairment infections chronic or family diseases etc.
……
……
……
……
……
……

TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER:
I certify that the above mentioned pupil is fit to pursue his/her Secondary Education.

Signature ……
Designation ……
Station ……
Date ……